# HOTUBA YA MWENYEKITI WA BODI YA CHUO CHA ARDHI MOROGORO PROFESA ……………… KWENYE MAHAFALI YA AROBAINI NA MOJA (41) YA CHUO CHA ARDHI MOROGORO TAREHE 14/04/2023

Mhe. Geophrey M. Pinda, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi;

Mh. Fatuma Mwassa, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro;

Bw. Seushi Mburi, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Ardhi Morogoro;

Bw. Charles Sospeter Saguda, Kaimu Mkuu wa Chuo cha Ardhi Morogoro;

Wajumbe wa Bodi ya Chuo cha Ardhi Morogoro;

Wakuu na Watendaji wote wa Taasisi na Idara za Serikali mliopo hapa;

Wajumbe wa Menejimenti ya Chuo cha Ardhi Morogoro;

Ndugu Wanahabari kutoka Vyombo Mbalimbali Vya Habari;

Wageni Waalikwa Wote, Mabibi na Mabwana,

**Habari za asubuhi!**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kwa niaba ya Bodi ya Chuo cha Ardhi Morogoro, Uongozi wa Chuo, Wanajumuiya na kwa niaba yangu binafsi, Napenda kuchukua nafasi hii, kuwakaribisha wote kwenye mahafali ya arobaini na moja (41) ya Chuo cha Ardhi Morogoro. **Karibuni sana!**

Aidha Napenda kuwashukuru wageni wote waalikwa kwa kukubali kujumuika nasi kwenye mahafali haya. Shukrani za pekee nazitoa kwako Daktari Angeline Mabula (MB), Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kukubali mwaliko wetu wa kuwa mgeni rasmi katika mahafali haya. **Asante sana**.

Vile vile nawashukuru wazazi, walezi, ndugu, jamaa, marafiki kwa kuwaleta vijana wenu kusoma hapa, kuwalipia ada na kama hiyo haitoshi mmetoa muda wenu na kushiriki katika sherehe hii muhimu ya kutunukia vyeti wahitimu wetu wa fani za Jiomatikia na Mipango Miji. **Asanteni sana.**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Pia, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati wahitimu wote **330** walioweza kumaliza masomo yao mwaka wa masomo 2021/2022 katika fani ya Upimaji Ardhi na Mipango Miji, ngazi ya Astashahada ya Awali, Astashahada na Stashahada ambao leo hii watatunukiwa vyeti vyao. Idadi hiyo inajumuisha wahitimu wa kike

**107 (32%)** na wahitimu wa kiume **223 (68%).** Aidha, kati ya wahitimu 330 watakaotunukiwa vyeti leo, **95 (29%)** wamesoma fani ya Mipango Miji ambapo wahitimu wa kike ni **37 (39%)** na wa kiume ni **58 (61%)**. Aidha, wahitimu **235 (71%)** ni wa fani ya Upimaji Ardhi ambapo wahitimu wa kike ni **70 (30%)** na wa kiume ni **165 (70%).**

**Wote hongereni sana.**

Nawatakia kila la heri katika ujenzi wa Taifa letu. Aidha nawashukuru sana wananchi na wadau wote wa ardhi kwa kuendelea kutumia huduma na ushauri unaotolewa na Chuo hiki katika nyanja za upangaji na upimaji ardhi, na uandaaji ramani za msingi kwa ajili ya makazi na matumizi mengineyo. **Asanteni sana.**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Majukumu ya Bodi ya Chuo cha Ardhi ni kusimamia, kushauri, kubuni mipango na kuhamasisha maendeleo ya Chuo. Majukumu mengine ya Bodi ya Chuo ni kuhakikisha wafanyakazi wanafanya kazi kwa bidii kwa kuzingatia dira, shabaha ya na malengo ya kuanzishwa kwa Chuo hiki.

Kwa nyakati tofauti Chuo kimeweza kutekeleza na kutafsiri kwa vitendo malengo ya kuanzishwa kwake. Mathalani, Chuo kimeweza kubadili mfumo wa mafunzo kukidhi matakwa ya soko na yale ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi. Vile vile Chuo kimeweza

kutekeleza Sera ya Taifa ya Ardhi kwa kutoa huduma ya kupima viwanja na mashamba katika halmashauri mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kwa kuzingatia mwelekeo uliopo wa mahitaji makubwa ya raslimali watu wenye ujuzi na weledi wa juu kitaifa na kimataifa, Chuo kimeandaa **Mpango Kabambe** unaoonesha mwelekeo wa ukuaji wa taasisi katika kipindi cha miaka ishirini (20) ijayo, yaani **2023 – 2043**. Mpango huu umelenga kukipanua Chuo kimiundombinu ili kuongeza udahili kutoka wanafunzi **496** waliopo sasa hadi kufikia wanafunzi **5250**; ambapo idadi ya wafanyakazi itaongezeka kutoka **45** walipo sasa hadi kufikia wafanyakazi **310** ifikapo mwaka **2043**.

Kadhalika, Chuo kinatekeleza Mpango Mkakati wa III wa Miaka Mitano (2022/2023 - 2026/2027) unaolenga kuiimarisha taasisi katika maeneo makuu manne: ubora wa elimu na wahitimu, vyanzo vya mapato, miundo mbinu ya kujifunzia na kufundishia, na usimamizi wa raslimali watu na raslimali fedha.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Ni matumaini yangu na Bodi ya Chuo kuwa utakuwa bega kwa bega nasi katika kusaidia utekelezaji wa mipango niliyoielezea hapo juu hususani kwa kupata wafadhili wa ndani na wa nje ya nchi ili kufanikisha utekelezwaji wa malengo ya Chuo chetu. Aidha nakuomba wewe binafsi uwe balozi wetu katika upanuzi wa Chuo

na kutafuta wafadhili kwa ajili ya masomo ya juu ya wakufunzi wetu.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Baada ya kusema haya, Napenda nihitimishe hotuba yangu kwa kukushukuru wewe binafsi na wageni wote waalikwa kwa kukubali mwaliko wetu. Nawashukuru Wajumbe wa Bodi kwa ushirikiano wao mzuri na Wanajumuiya ya Chuo cha Ardhi Morogoro walioshiriki kwa njia moja au nyingine katika kufanikisha Mahafali haya. Mwisho nakuomba kwa heshima na taadhima kubwa utumie fursa hii kuongea na hadhara iliyopo mbele yako na baadaye uwatunuku vyeti wahitimu **330** wa fani za Upimaji Ardhi na Ramani na wahitimu wa fani ya Mipango Miji na Vijiji wa Chuo cha Ardhi Morogoro.

**Asanteni kwa kunisikiliza na Karibuni sana.**